# HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU

## Nanenane 2023

MERU DC KAZI IENDELEE | KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI | JARIDA LA NANENANE





# NANENANE 2023

Imeandaliwa na Kutolewa na:
Kitengo Cha Mawasiliano Serikalini
Halmashauri ya Wilaya ya Meru

Mhariri Mkuu: Zainabu J Makwinya
Mhariri Msaidizi: Annamaria Makweba
Msanifu wa Jarida: Ludovick Mkenda
Msanifu Msaidizi: Isaya Sango

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Meru
S.L.P 462, Usariver
Simu: +25527297082
Barua pepe : ded@merudc.go.tz
www.merudc.go.tz

# UTANGULIZI

Nane nane ni Siku ya wakulima nchini Tanzania ambayo huwapa fursa wakulima, taasisi na wadau mbalimbali wa kilimo kote nchini Kuonesha bidhaa zao na mafanikio yao katika mwaka husika.

Mwanzo sikukuu hii ya nane nane iliitwa 'Saba Saba' ambapo ilikuwa ikiadhimishwa kila tarehe 7 ya mwezi wa Julai. baadaye ilihamishiwa Agosti, 8 ya kila mwaka baada ya saba saba kufahamika zaidi kwa maonyesho ya wafanyabiashara.

Sikuu kuu ya maonyesho ya wakulima iliadhimishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1977 ili kuongezea nguvu sera ya Serikali ya wakati huo ya 'siasa' ni Kilimo ambapo wakulima katika Wilaya mkoa na taifa walionesha mazao yao halisi ya kilimo pamoja na kufundishwa namna ya kutumia pembejeo za kilimo kwa ustawi wa Taifa.

Mwaka 2023 maonesho ya nane nae kwa kanda ya Kaskazini yamefanyika katika mkoa wa Arusha ambapo wilaya mbalimbali na halmashauri zake zilishiriki katika kuonesha mbinu mbaalimbali zinazotumika katika kilimo na ufugaji

Halmashauri ya wilaya ya Meru ni miongoni mwa Halmashauri zilizoshiriki katika maonesho ya nanenene yaliyofanyika katika viwanja vya Themi Njiro.

Halmashauri ya Meru imeonesha uwezo mkubwa kupitia wananchi wake ambao ni wakulima na wafugaji ujuzi elimu na mbinu mbalimbali zinazotumika katika kilimo na ufugaji, watalamu mbalimbali wameshiriki katika kutoa elimu wananchi walishiriki katika maonesho hayo ya kilimo na ufugaji

Mpendwa Mkulima na Mfugaji wa jarida hili la nane nane karibu ujionee mbinu mbalimbali zinazotumika katika kilimo. katia jarida hili tumekuandalia mchakato mzima unaofanyika kwanzia shambani hadi sokoni.

Tutajionea wakulima wanavyofanya kazi hadi uzalishaji. katika wilaya ya Arumeru tunao wakulima wa nyanya, miche ya matunda mbalimbali, kilimo cha mbegu za matunda mbogamboga, mahindi n.k

Katika ufugaji tutaangazia zaidi ufugaji wa Ng'ombe wa maziwa mengi, Kuku wa nyama na mayai, bata, mbuzi n.k

Utaalamu na dondoo mbalimbaii Tumeongozwa na asfisa kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Meru Digna Massawe karibu ujifunze .



# UFUGAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA WILAYA YA MERU



Mjasiriamali Emanuel Nanyaro mkazi wa wilaya ya Meru anaejishughulisha na ufugaji wa ng'ombe wa wa maziwa aina ya Freisian na Ashley , ameeleza kuwa anauzoefu wa ufugaji wa ng'ombe wa maziwa zaidi ya miaka 13 akiwa na mbinu tofautitofauti za za ufugaji na mbegu za kisasa za kuzalishia ng'ombe hao wa maziwa. Pia ameeleza kuwa aina hiyo ya ng'ombe anayofuga huweza kutoa lita 40 kwa siku ambayo humwezesha kupata kipato cha kutosha kujikimu Katika maisha yake ya kila siku. Ng'ombe hao wanauwezo wakutoa maziwa mengi kwa siku kwasababu ya mbegu bora kutoka kituo cha uzalishaji wa mbegu za ng'ombe NAIC inayopatikana katika wilaya ya Meru, pili ni namna ya ulishaji wa ng'ombe ambapo ameeleza yeye analisha ng'ombe wake vizuri kwenye viwango vinavyotakiwa.



# Mradi wa kilimo cha mbogamboga na matunda na mjasiriamali Joram Mbuza







Mjasiriamali huyu hujihusisha na kilimo cha kisasa kwa kutumia Greenhouse ambapo huzalisha miche bora na kuuzia kampuni za maua. Katika kupata mishe bora hutumia mbinu ya upandikizaji wa mbegu (Crossbreeding) ambapo huchukua takribani miezi mitatu ili matunda yaive ili kuvunwa kupata mbegu. "Kazi yetu ni kuzalisha mbegu kwaajili ya kuuzi kampuni za maua, kwaiyo kampuni za maua zinatuletea mbegu yakiume na kike tunapanda hizo mbegu alafu tunachukua yale maua ya kike na kiume tuna cross(kupandikiza) na zile mbegu zinazopatikana baada ya hapo ndio tunawauzia". Lakini pia mjasiriamali huyu huzalisha hoho za rangi ya njano na nyekundu. Ambapo ameeleza sababu ya kulima hoho za rangi ya njano na nyekundu ni kuwa hoho za rangi hulipa sana sokoni tofauti na zile za rangi ya kijani, akaongeza kusema kuwav katika lishe hoho zote zina lishe sawa utofauti ni rangi tu kuwa zile za rangi ya njano na nyekundu huvutia wateja na soko kubwa la hoho anazozizalisha ni hoteli kubwa.

# Ufugaji wa kuku wa mayai na ndugu Joram Mbuza

Ndugu JORAM MBUZA mkazi wa wilaya ya Meru kata ya Kikwe, kijiji cha Nambala ambaye ni mjasiriamali anayejishughulisha na kilimo cha kisasa cha biashara pamoja na uzalishaji wa mazao na miche ya mbogamboga na matunda, na pia ni mfugaji wa kuku wa kisasa wa mayai. Ndugu Joram Mbuza anajihusiha na ufugaji wa kuku wa kisasa wa mayai akiwa na jumla ya kuku wa mayai 700 ambapo hununua kutoka katika kampuni ya INTERCHIK na kuwakuza kwa kuhudumia mwenyewe katika makazi yake kwa ajili ya kujipatia kipato. Aidha mjasiriamali huyu ameeleza kuwa katika kupata kuku bora wa mayai hutumia mbinu za kisasa za ufugaji kama kuweka kwenye mashine maalumu ya makuzi kwa kuzingatia ukubwa wa chumba cha makuzi na njia bora kuepusha na magonjwa nyemelezi kwa kuku na pia hutumia vyakula vya kisasa kama Brower , Stata na hutumia mimea maalumu aina ya LUSERN yenye protein yakutosha kwa ajili ya kuongeza protini yakutosha kwa kuku hao ambapo huchukua miezi mitano mbaka kuku hao waanze kutaga mayai. "Hawa ni kuku wa kisasa na ukiwalisha vizuri kama kilo 20 mbaka 25 ni kama asilimia 85 hivi wanaotaga, sio rahisi kuku wote wanaweza kutaga siku hiyo kuna wengine wanapumzika kidogo mfano ukiwatunza vizuri ndiyo, asilimia ya kutaga inazidi kupanda". Pia ndugu Joram katika ufugaji wa kuku wa kisasa wa mayai ameeleza kukumbana na changamoto mbambali ambapo changamoto kubwa ni upatikanaji wa chakula ambacho kimetengenezwa na makampuni mbalimbali ambapo huuzwa kwa gharama kubwa inayoleta changamoto kwa mfugaji kuweza kununua.

Lakini ameeleza kuwa ili kutatua changamoto hiyo ya chakula kuwa bei ya juu sana hutumia njia mbadala kwa kununua na kuchanganya vyakula tofauti tofauti kwa kufuata ushauri wa wataalamu mbalimbali ili kupa chakula chenye ubora wakutosha ili kupata mayai mengi.





# MKULIMA WA NYANYA PETER NNKO

Mkulima wa nyanya kutoka kijiji cha Maji ya Chai katika halmashauri ya wilaya ya Meru atoa ushuhuda jinsi kilimo hicho kilivyomsaidia kijikwamua kimaisha na kuweza kuihudumia familia yake, pia kuendesha maisha yake ya kila siku, pia ameeleza kuwa na uzoefu wa zaidi ya miaka miwili katika ukulima wa nyanya huku akimshukuru afisa kilimo wa kata Ndugu Jonathan kwa kumsaidia katika ushauri uliomfanya aweze kufanya kilimo chenye tija na faida kubwa kuweza kujiajiri. Aidha ndugu,Peter aeleza faida za kilimo hicho cha nyanya jinsi kilivyo badilisha maisha yake na kupata mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kumwezesha kusomesha watoto wake na kumfanya ajivunie kwa kiasi kikubwa kuwa mkulima wa nyanya. Vilevile ametoa maoni kwa wakulima wengine kuzingatia mbinu bora za kilimo ili kufanya kilimo chenye manufaa kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu na pia amewaasa wakulima wa nyanya kuzingatia mbegu bora ambazo zitazoweza kuongeza uzalishaji wakutosha na kuwapa faida. Kuelekea sikukuu ya wakulima (Nanenane) ndugu Peter Nnko amewakaribisha wakulima wenzake wa nyanya kuhudhuria maonesho hayo ili kuona jinsi wakulima wengine wanyanya walivyoweza kuwa mfano wakuigwa kutokana na kuzalisha nyanya bora









# MZALISHAJI WA MICHE BORA YA KISASA YA MATUNDA









Mjasiriamali Emmanuel Victor Tushare mkazi wa Tengeru wilaya ya Meru mwenye taaluma ya Agricultural product ambaye anajishughilisha na uzalishaji wa miche bora ya kisasa ya matunda naya muda mfupi akitumia mtindo wa budding and crafting. Hujishughulisha na uzalishaji wa matunda ya kisasa kama vile parachichi, maembe, mastafeli n.k. Aidha ameeleza hatua za uandaaji wa miche hiyo ambapo kwa kuanza na kusia mbegu kwenye ardhi ambapo huchukua mwez mmoja hadi mbegu hiyo kuota na pia huchukua mwezi mwingine mmoja kutegemana na mche ili kufikia hatua ya kuweza kukatwa na kuungwa ili kupata mche kamili. Katika kutumia mtindo wa budding na crafting hutegemeana na aina ya tunda ambapo kwa matunda kama parachichi hutumia crafting lakini kwa miche kama limao, chungwa, ndimu wanatumia budding na miche kama zabibu hutumia cutting, ili kuunga miche hiyo huusisha kuunga kati ya mtishina na kikonyo. Pia namna wanavyopata masoko ya miche ameeleza kuwa wana. ungana na taasisi za kilimo na pia wanazunguka kwa wakulima ili kutoa elimu kuhusiana na miche ya kisasa ya matunda, mbali na masoko pia wamekua wakitoa elimu juu ya umuhimu wa afya katika jamii, na pia huunda vikundi mbalimbali vya wakulima wa matunda ambapo kupitia viongozi wa vikundi hivyo hujipatia wateja Pamoja na juhudi zake katika kuzalisha miche bora ya matunda ameeleza pia kuwa serikali imechangia kwa kiasi kikubwa kwa

Lakini pia mjasiriamali huyu ame kuwapa mafunzo hususani zao la parachichi na pia walipewa vyeti vya kuhitimu mafunzo hayo na pia serikali imetoa ahadi ya kuwasaidia katika kutafuta masoko kwa kuweka sheria itayowasaidia kuuza miche hiyo kupitia nembo ya TOSKI ambayo itasaidia kuthibitisha kuwa miche inayouzwa kuwa halisi. toa kwa ufupi changamoto ambazo hukabili kilimo hichi cha miche ya matunda ambapo ameeleza kuwa changamoto kuu ni hali ya hewa ambayo hufanya mbegu kuchelewa kukua hasa katika kipindi cha baridi tofauti na kipindi cha joto ambapo miche hukua kwa kasi. Mwisho ndugu Emanuel ameeleza kuwa upandikizaji wa miche ya matunda tofautitofauti una una faida kubwa kwani husaidia kupata miche ya matunda ambayo huzaa baada ya muda mfupi ukilinganisha na mti ambao haujapandikizwa, mfano mti uliopandikizwa unaweza kuchukua miaka miwili na nusu kutoa matunda lakini mti ambao haujapandikizwa huchukua maika 8 hadi 10 ili kuweza kuzaa matunda








# UZALISHAJI NA UUZAJI WA ASALI KATIKA WILAYA YA MERU NA KIKUNDI CHA GOLDEN HEART










Pantaleo Nestory Mgala katibu wa kikundi cha Golden heart kinachijishughulisha na uzalishaji na uuzaji wa bidhaa itokanayo na nyuki, pia ni moja ya kikundi kilichonufaika na mkopo kutoka katika wilaya ya Meru wakifanikiwa kupata kiasi cha shilingi milioni 7 iliyofanikisha kufikia malengo ya kupanua biashara yao itokanayo na ufugaji wa nyuki na usambazaji wa bidhaa zitokanazo na nyuki. Pia ameeleza jinsi gani wamenufaika na biashara hiyo wakiwa katika kikundi cha watu 15 ikiwa ni ajira yao inayowapatia kipato na pia imewanufaisha watu wengine wanaowazunguka kwa kuwapa ajira kutokana na kununua bidhaa hiyo kwa jumla na kuzisambaza rejareja kwa watumiaji pia ameendelea kusema wamenufaika kwa kujitengenezea vifaa vyao wenyewe vya uzalishaji wa asaliss

# PICHA MBALIMBALI ZA WAKULIMA NA WAFUGAJI KWENYE MAENEO YAO YA UZALISHAJI













Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, S.L.P 462, Usa River, Arusha, simu +255272970482, Barua pepe: ded@merudc.go.tz, www.merudc.go.tz

# YALIYOJIRI WAKATI WA MAADHIMISHO YA SIKU YA NANENANE



*Ndugu mpenzi mfuatiliaji wa Jarida hili Maalumu la Nanenane 2023, Baada ya kuona yanayofanyika Shambani na wakulima pamoja na Wafugaji Sasa Tuangazie yaliyojiri siku ya Maadhimisho ya Nanenane ambapo kwa Knda ya Kaskazini yamefanyika Mkoa wa Arusha na kufunguliwa na Spika wa Baraza la wawakilishi Zanzibar, Mhe. Zuber Ali Maulid katika viwanja vya Themi Njiro*



kanguvukubwakatikakuboresha kilimo na mifugo amba Maonesho ya wakulima na sikukuunya nanenane mwaka 2023 yamezinduliwa tarehe 03.08.2023 na spika wa Baraza la wawakilishi Zanzibar4, Mhe. Zuber Ali Maulid katika viwanja vya Themi njiro Maonesho haya kwa mwaka 2023 ni maonesg ya 29 kitaifa, ambapo kwa mwaka 2023 maonesho haya yamekuwa na hamasa kubwa kwa kanda ya kaskazini ukilinganisha na miaka ya nyuma kutokana na wingi wa watu kujitokeza kushiriki katika maonesho haya po mikoa ya kanda ya kaskazini imefunika na utoaji wa mbolea ya ruzuku kwaajili yankuongeza tija kwenye kilimo ambapo kw mwaka 2022/2023 jumla ya tani 17,288 zimetolewa kwa mkoa wa Arusha na kuwanufaisha wakulima 19,633, tani 18557 zimetolewa kwa mkoa wa Kilimanjaro na kuwanufaisha wakulima 62,829 tani 4,840 zimetolewa kwa mkpa wa Manyara na wakulima 62,826 wamenufaika. Moja kati ya mambo yaliyoelezwa na Mhe. Zuber Ali Maulid katika uzinduzi wa maonesho hay ani pamoja na sekta za kilimo, Mifugo na Uvuvi kuwqa ni mchango mkubwa katika pato la taifa kwa uchumi wa mwananchi mmoja mmoja kwani Zaidi ya asilimia 90% ya wanachi wa kanda ya kaskazini kwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara wanajihusisha na shughuli za kilimo mifugo na uvuvi. Kwa takwimu ambazo Mhe. Zuber Ali Maulid amezitoa katika hotuba yake ni kwamba, kwa mwaka 2022/2023 serikali imewea idha, ameeleza kuwa serikali imetoa Pikipiki kwa maafisa ugani ili kuwezesha kufanya shughuli za ugani kiurahisi na kuwafikia wakulima wengi Zaidi ambapo Pikipiki 245 zimetolewa kwa Mkoa wa Kilimanjaro, 151 zimetolewa kwa mkoa wa Manyara na 210 zimtolewa kwa mkoa wa Arusha. Vilevile, Mhe, zuber ameeleza kuwa, Maonesho haya yana lengo la kuonesha fursa zilizopo katika sekta za kilimo, Mifugo na Uvuvi na kutoa elimu kwa wakulima, wafugaji na wavuvi ili uzalishaji wa mazao na bidhaa zizatoka kwenye sekta hizo yawe na tija na hatimaye kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Nchi yetu ya Tanzania.

# Baadhi ya Picha za Matukio Mbalimbali Siku ya Nane nane





Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl. Zainabu J. Makwinya akiwa na kikundi cha Vijana waliopata ufadhili kutoka Shirika lisilo la Kiserikali linalojishughulisha na masuala ya Kilimo katika Halmashauri ya Meru Rikolto alipotembelea banda la Halmashauri ya Meru katika Maonesho ya Kilimo Nane nane viwanja vya Themi Njiro



Pichani ni washindi wa Tatu Halmashauri ya Wilaya ya Meru katika Maonesho ya Nane nane Kanda ya Kaskazini 2023



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Meru Mwl. Zainabu J. Makwinya akiwa kwenye banda la Bi Elinuru N. Urio na Kupata elimu juu ya zao la Kweme












# RC- MANYARA-MHE. QUEEN SENDIGA "ELIMU YA WAKULIMA ITOLEWE KWENYE MAENEO YAO"

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mhe. Queen Sendiga amewataka wataalam wa Kilimo na Mifugo kwenda kutoa elimu katika maeneo ya wafugaji na wakulima kama ambavyo wamefanya katika maonesho ya Nane nane.

Ametoa rai hiyo siku ya kilele cha maonesho ya 29 ya Nanenane Kwa Kanda ya Kaskazini yaliyofanyika katika viwanja vya Themi Njiro Mkoani Arusha " Nitoe rai kwa Wataalam wa Kilimo, Maafisa Kilimo, Madaktari wa Mifugo, Mabi bi Lishe na Maafisa Afya, kwa namna ambavyo mmejipanga kwenye mabanda kwa wiki yote ya nanenane kuhakikisha mnatoa elimu ipasavyo, ndiyo namna hii hii tuenende tukafanye kwenye maeneo yetu" Alisema Mhe. Sendiga.

Aidha, Mhe. Sendiga amesisitiza kuwa ushuru unaokusanywa kwenye mazao ya kilimo na mifugo, asilimia 5 iwe inarudi kwenye maeneo husika Kwa ajili ya kuboresha maeneo hayo. Vile vile, Mkuu huyo amesisitiza Kuhusu kilimo na Ufugaji wa Kisasa kwa wakulima na wafugaji ili kukabiliana na upungufu wa maeneo ya malisho lakini kuweza kusaidia Taifa kuondokana na janga la uharibifu wa mazingira kulingana na hali ya mabadiliko ya tabia ya Nchi.

Maonesho ya 29 ya Wakulima kanda ya Kaskazini yamehusisha Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara ambapo Kitaifa maonesho hayo yamefanyika Mwakangale Mkoani Mbeya.









Pichani ni Mwakilishi wa Rikolto akpokea Cheti Cha Ushindi kwenye maadhimisho ya Nanenane

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, S.L.P 462, Usa River, Arusha, simu +255272970482,
Barua pepe: ded@merudc.go.tz, www.merudc.go.tz

# PICHA MBALIMBALI ZA MATUKIO KWENYE WIKI YA NANENANE 2023











Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya, Halmashauri ya Wilaya ya Meru, S.L.P 462, Usa River, Arusha, simu +255272970482, Barua pepe: ded@merudc.go.tz, www.merudc.go.tz

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MERU



## “Vijana na Wanawake ni msingi imara wa mifumo endelevu ya Chakula”

## JARIDA MAALUMU LA NANE NANE 2023

HALMASHAURI YA WILAYA
MERU
DISTRICT COUNCIL